



# SHIRIKA LA DAMU TAKATIFU YA YESU

SOCIETY OF THE PRECIOUS BLOOD



## MAISHA YA MTAKATIFU GASPARI

Mtakatifu Gaspari Del Bufalo alizaliwa Roma tarehe 6.1.1786. Akiwa bado mdogo alikuwa anaamshwa na wokovu wa watu hadi akajaribu kutoroka nyumbani na kwenda kuwatangazia wapagani imani.

Katika ujana wake alikuwa mfano bora wa usafi wa moyo, uchaji na Ibada. Alipopata upadre alianza kazi yake kati ya mapadre na kati ya masikini na wagonjwa. Roma ilipovamiwa na Napoleone, Mt. Gaspari alikataa kuapa mbele ya mwakilishi wake akisema "sipaswi, siwezi na sitaki." Alikubali kwenda utumwani na kufungwa gerezani. Alipokuwa gerezani alipata wazo la kuanzisha shirika la mapadre na masista wa Damu Takatifu ya Yesu.

Alipoachiwa huru mwaka 1815 tarehe 15 mwezi wa nane alianzisha shirika la mapadre wa Damu Takatifu ya Yesu. Pamoja na Mt. Maria De Mattias akaanzisha shirika la masista waabuduo Damu Takatifu ya Yesu kazi kubwa pamoja na mapadre wengine ilikuwa ni kwenda kila mahali kutoa mafungo kwa Wakristo wa kawaida. Kwa mahubiri yake wengi walifaidika na Mungu alikuwa anayabariki kwa miujiza mbalimbali. moyo wake ulimsukuma mpaka katikati ya majambazi ili aweze kuwarudisha kwa Mungu na kwenye jumuiya ya watu. Maisha ya Mt. Gaspari hayakuwa marefu sana kwa sababu ya masumbufu na taabu nyingi alizovumilia. Mungu alimchukua tarehe 28. 12. 1837 akiwa na umri wa miaka 52. Alitangazwa kuwa Mtakatifu na Baba Mtakatifu Pius 12 tarehe 12. 6. 1954.

## NA WEWE JE?

Ungependa kujiunga nasi?  
Iwapo unafikiri kuwa umeitwa na Mungu  
kuwa Padre au Bruda, kwa kujua zaidi  
andika kwa:

Mkurugenzi wa Miito  
Shirika la Damu Takatifu ya Yesu,  
S.L.P 3086  
Dododma - Tanzania  
E mail: [vdpreciousblood.tz@gmail.com](mailto:vdpreciousblood.tz@gmail.com)  
Mobile: 0757 213 226  
Tovuti: [WWW.cppstanzania.com](http://WWW.cppstanzania.com)

“Ningependa kujua Lugha  
elfu na kuwa na moyo  
uliojaa upendo wa Damu  
Takatifu ya Yesu ili  
niwaangazie watu wote  
habari njema ya  
ukombozi.”

Mt. Gaspari